Musa

na

Ellis P. Forsman

Musa

na

Ellis P. Forsman

Oktoba 13, 2011

Musa

Waebrania 11:23-29

Musa alikuwa ni mmoja katika ya watu wenye tabia kuu katika Agano la Kale. Kumb. 34:10, "*Wala hajainuka tena katika Israel nabii kama Musa, ambaye BWANA alimjua uso kwa uso.*"

Ni mfano mkuu kati ya wanadamu wote wa historia yote.

Jina lake linaonekana katika Biblia zaidi ya mara mia saba na hamsini ndani ya vitabu thelathini vya Biblia.

Musa alikuwa mwandishi (aliandika vitabu vitano vya kwanza vya Biblia), mtoa sheria, mjenzi wa hema, nabii, mpatanishi, na mfano wa Kristo.

Musa alikuwa "rafiki wa Mungu". Kut. 33:11, "*Naye BWANA akasema na Musa uso kwa uso kama vile mtu asemavyo na rafiki yake…*"

Alichaguliwa kuwatia imani watu. Ebr. 11:23-29, "*Kwa imani Musa alipozaliwa, akafichwa miezi mitatu na wazazi wake kwa sababu waliona kuwa alikuwa mtoto mzuri; wala hawakuiogopa amri ya mfalme. Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo. Kwa imani akatoka Misri asiogope ghadhabu ya mfalme maana alistahimili kama amwonaye yeye asiyeonekana. Kwa imani akaifanya pasaka na kule kunyunyiza damu, ili yule mwenye kuwaangamiza wazaliwa wa kwanza asiwaguse wao. Kwa imani wakapita kati ya Bahari ya Shamu, kama katika nchi kavu; wamisri walipojaribu kufanya hivyo wakatoswa.*"

Miaka arobaini ya Musa

Musa alizaliwa katika nyakati za hatari. Ulikuwa ni wakati ambapo Farao aliinuka na hakumjua Yusufu. Kut. 1:8, "*Basi akainuka mfalme mpya kutawala Misri asiyemjua Yusufu.*"

Israeli walikuwa Misri kwa miaka mia nne. Idadi yao imekuwa kutoka sabini hadi labda wengi kama milioni mbili. Wanaongezeka katika nchi. Kut. 1:7, "*Na wana wa Israeli walikuwa na uzazi sana, na kuongezeka mno, na kuzidi kuwa wengi, nao wakaendelea na kuongezeka nguvu na ile nchi ilikuwa imejawa na wao.*"

Wamisri waliogopa kwamba kama wakienda vitani, Israeli watawaungana na maadui zao. Kut. 1:10, "*Haya na tuwatendee kwa*

akili wasije wakaongezeka tena ikitokea vita wao nao wasije wakashikamana na adui zetu na kupigana nasi na kutoka katika nchi hii."

Hivyo Farao akawatuma wakuu wa ushuru ili kuongeza mzigo kwa Waisraeli. Vile vile, zaidi ambavyo Waisraeli walivyopokea mizigo hii, ndivyo walivyoongezeka! Kut. 1:11, "*Basi wakaweka wasimamizi juu yao wawatese kwa mizigo yao. Nao wakamjengea Farao miji ya kuwekea akiba, Pithomu na Ramesesi.*"

Kisha Farao akawaagiza wazalisha kuwaua watoto wote wa kiume wa Kiebrania. Wasinge fanya hivyo kwa kumwogopa Mungu. Kut. 1:15-21, "*Kisha mfalme wa Misri akasema na wazalisha wa Waebrania, mmoja jina lake aliitwa Shifra, na wa pili jina lake aliitwa Pua; akasema wakati mwazalishapo wanawake wa Kiebrania na kuwaona wa katika kuzaa, ikiwa ni mtoto mwanamume, basi mwueni, bali ikiwa ni mtoto mwanamke, na aishi. Lakini wale wazalisha walikuwa wakimcha Mungu, wasifanye kama walivyoamriwa na huyo mfalme wa Misri, lakini wakawahifadhi hai wal wanaume. Basi mfalme wa Misri akawaita wale wazalisha na kuwauliza, kwa nini kufanya jambo hili, na kuwahifadhi watoto waume wawe hai? Wazalisha wakamwambia Farao ni kwa sababu hao wanawake wa Kiebrania si kama wanawake wa Kimisri kwa kuwa ni hodari hao, nao huzaa kabla mzalisha hajapata kuwafikilia. Basi Mungu akawatendea mema wale wazalisha na hao watu wakaongezeka sana, wakaendelea na kuzidi kuwa na nguvu nyingi. Ilikuwa kwa sababu wale wazalisha walikuwa wakimcha Mungu, akawasimamishia nyumba.*"

Kisha Farao akaagiza kwamba watoto wote wa Kiebrania watupwe mtoni. Kut. 1:22, "*Kisha huyo Farao akawaagiza watu wake, akisema kila mtoto mwanaume atakayezaliwa mtamtupa mtoni, na kila mtoto na kila mtoto mwanamke mtamhifadhi hai.*"

Wazazi wa Musa.

Walikuwa ni Amram na Yoshebeli. Wote walikuwa wa kabila la Lawi. Kut. 2:1, "*Mtu mmoja wa nyumba ya Lawi akaondoka akaona binti mmoja wa Lawi.*"

Musa alipozaliwa alikuwa mtoto mwema. Mdo. 7:20, "*Wakati huo akazaliwa Musa, naye alikuwa mzuri sana akalelewa muda wa miezi mitatu katika nyumba ya babaye.*"

Moja kati ya mistari mikuu katika Biblia ni Ebr. 11:23, "*Kwa imani Musa alipozaliwa akafichwa miezi mitatu na wazazi wake, kwa sababu waliona kwamba ni mtoto mzuri; wala hawakuiogopa amri ya mfalme.*"

Ni imani iliyoje na ujasiri ulioonyeshwa na wazazi wa Musa! Bila kujali aligeuka kama alivyofanya.

Lakini wakati ulifika ambapo Musa asingeweza kufichwa tena. Hivyo kikapu cha ukindu kilitengenezwa. Labda wazazi wa Musa waliamini kwamba mtoto wao atakuwa salama mtoni. Asingeweza kupatikana pale. Wakaweka kikapu hicho kisichoingiliwa na maji katika mto Nile. Labda waliamini kwamba binti Farao atamwokota na kwa sababu ya uzuri wake, wakamwacha hii ilitokea kwa msaada wa Mungu. Miriamu dada yake, aliruhusiwa kuchagua mzalisha wa Kiebrania, na akamchagua mama yake Musa mwenyewe kumwangalia.

Kut. 2:7-10, "*Basi umbu lake mtoto akamwambia binti Farao, Je! Niende nikamwite mlezi katika wanawake wa Kiebrania, aje kwako, akunyonyeshee mtoto huyu? Binti Farao akamwambia haya enenda. Yule kijana akaenda akamwita mama yake yule mototo. Binti Farao amwambia mchukue mtoto huyu ukaninyonyeshee, nami nitakupa mshahara wako. Yule mwanamke akamtwaa mtoto, akamnyonyesha. Mtoto akakua naye akamleta kwa binti Farao, akawa mwanawe. Akamwita jina lake Musa, akasema, ni kwa sababu nalimtoa majini.*"

Binti Farao alimwita Musa ikimanisha "kuchukuliwa kuoka majini." Hivyo, mama yake Musa mwenyewe alirurhusiwa kumnyonyesha wakati wa miaka hiyo muhimu. Amrani na Yoshebeli wanatuonyesha kwamba mila aihitaji kuharibu roho ya kichanga. Hata kama alilelewa kati ulimwengu wa kipagani, Musa, kama tutakavyoona, alishikilia vyema imani yake katika Mungu mmoja wa kweli na anayeishi.

Kumb. 6:4-9, "*Sikiza, Ee Israeli; BWANA Mungu wetu, BWANA ndiye mmoja. Nawe mpende BWANA Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa nguvu zako zote. Na maneno haya ninayokuamru leo, yatakuwa katika moyo wako; nawe uwafundishe watoto wako kwa bidii, na kuyanena uketipo katika nyumba yako, na utembeapo njiani, na ulalapo, na uondokapo. Yafunge yawe dalili juu ya mkono wako, nayo yatakuwa kama utepe katikati ya macho yako. Tena yaandike juu ya miimo ya nyumba yako, na juu ya mlango wako.*"

Miaka arobaini ya pili ya Musa

Kadiri miaka ilivyoendelea, Musa alikua. Mdo. 7:20-22, "*Wakati huo akazaliwa Musa, naye alikuwa mzuri sana akalelewa muda wa miezi mitatu katika nyumba ya babaye. Hata alipotupwa, binti Farao akamtwaa akamlea awe kama mwanawe. Musa akafundishwa hekima yote ya Wamisri, akawa hodari wa maneno na matendo.*"

Tayari tumeshaongelea mtazamo wa Musa. Hakuna shaka kwamba alikuwa kijana mzuri. Lazima alikuwa amebarikiwa na vitu vingi vya kimwili. Haya yanasaidia, lakini mara nyingi siyo muhimu kwa mafanikio. Mungu haangalii utu wa nje, bali ndani ya moyo. 1 Sam.

16:7, "*Lakini BWANA akamwambia Samweli, usimtazame uso wake, wala urefu wa kimo chake; kwa maana mimi nimemkataa. BWANA haangalii kama binadamu aangaliavyo; maana wanadamu hutazama sura ya nje, bali BWANA huutazama moyo.*"

Musa alikuwa jitu lenye nguvu. Baada ya yote, alikuwa ni kijana wa binti Farao. Alilelelwa katika nyumba ya kifalme. Alikuwa na elimu nzuri katika ulimwengu. Alifundishwa vitu kama sayari, nyota, hesabu, madawa. Hakuna shaka kwamba, alifundishwa mifumo ya kijeshi na jinsi ya kupigana.

Musa pia alikuwa kiongozi. Yosephus alisema kwamba wakati Misri ilipovamiwa na Wahabeshi, Musa alikuwa jenerali na akaongoza Misri katika ushindi.

Wakati ulifika ambapo Musa alijifunza kwamba kulikuwa na zaidi katika maisha kuliko kile alichokifahamu.

Labda Musa ni mfano mzuri wa kauli ya Sulemani, ukimlea mtoto katika njia nzuri, hataiacha (Mith. 22:6). Hapa pia kuna maelezo mazuri ya ukweli kwamba uzima wa mtu haujumuishi wingi wa vitu alivyonavyo (Luka 12:15).

Hakuna msitari katika Biblia nzima unaoeleza zaidi mabadiliko yaliyomtokea Musa kuliko Ebr. 11:24-26, "*Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima akakataa kuitwa mwana wa binti Farao; akaona ni afadhali kupta mateso pamoja na watu wa Mungu kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo; akihesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri; kwa kuwa aliyatazamia hayo malipo.*"

Hakika, huu ulikuwa maamuzi yakuumiza kwa Musa. Kimsingi alimpenda binti Farao. Binti huyu alimfanyia mengi. Hataivyo unaiangalia, maamzi yake yalikuwa dhabihu binafsi. Alikuwa na hekima, heshima, na bahati. Bado, aliyatoa yote katika maisha ya mateso, tiba ya maradhi na mateso.

Musa anawezaje kufanya uamuzi kama huo?

Musa alitambua kwamba raha ya dhambi hufika tamati kwa kitambo. Hakika, nahisi kwamba Musa alitambua kwamba dunia ilikuwa inapita, na maisha katika urefu wake ni mafupi hakika.

- Zaburi 90:10, "*Siku za miaka yetu ni miaka sabini, na ikiwa tuna nguvu miaka themanini; na kiburi chake ni taabu na ubatili, maana chapita upesi tukatokomea mara.*"
- Yak. 4:14, "*walakini hamjui yatakayokuwako kesho. Uzima wenu ni nini? Maana ninyi ni mvuke uonekanao kwa kitambo, kisha hutoweka.*"

Musa pia alitambua kwamba heshima yake, utukufu, umaarufu, uwezo, na utajiri ungeishia katika matukio ndani ya kifo na katika umilele. Kifo ndiyo hitimisho kuu.

Musa aliamini kwamba mateso na tiba ya ugonjwa au dhiki kama ile aliyobeba Yesu ingemwezesha kuweka hazina yake mbinguni.

Mat. 6:19-21, "*Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba; bali jiwekeeni hazina mbinguni, kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu, wala wevi hawavunji wala hawaibi; kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako.*"

Musa alitunza zawadi ya uzima kila mara mbele yake. Aliangalia mbele ya maisha haya hadi nyingine. Alizingatia uzima wa milele kuwa ni muhimu sana kuliko maisha yake ya duniani. Mungu ni Mungu anaelipa. Ebr. 11:6, "*Lakini pasipo imani haiwezekani kumpendeza maana mtu amwendeaye Mungu lazima aamini kwamba yeye yuko na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao.*"

Zawadi ya umilele yetu inapaswa kututia changamoto kutafuta vitu vilivyoko juu na siyo vitu vilivyoko duniani. Kol. 3:1-2, "*Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu siyo yaliyo katika nchi.*"

Mwisho, Musa aliweka macho yake kwa Mungu anayeonekana. Hii ilimwezesha kuvumilia. Wakristo wanaambiwa "*…na tupige mbio kwa saburi katika yale mashindano yaliyowekwa mbele yetu; tukimtazama Yesu, mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu, ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu.*" (Ebr. 12:1-2).

Kama tutaweka macho yetu kwa Mungu kupitia imani. Hii ilimwezesha kushinda kikwazo cha aina yo yote katika maisha ambayo hayakuwa mazuri.

Muda ulifika ambapo maisha ya Musa yalimshinikiza kuchagua kati ya kimwili na kiroho. Sisi pia lazima tufanye uchaguzi.

Yesu alisema katika Mat. 6:24, "*Hakuna mtu awezaye kutumikia mabwana wawili, kwa maana atamchukia huyu na kumpenda huyu, na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali.*

- Mat. 6:33, "*Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa.*"
- Mat. 16:24, "*Wakati huo Yesu aliwaambia mtu ye yote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake anifuate.*"

Musa alikuwa na muda enzi za uhai wake alipofanya kila kitu sahihi. Pia alikuwa na muda katika maisha yake alipofanya makosa makubwa.

Je umewahi kufanya kosa hadi dunia yote ikaoneka kwamba iko kinyue na wewe? Musa alifanya. Alafu, Mungu anamtumia Musa bila kujali makosa yake. Mungu hakumgeuzia mgongo.

Katika Kut. 2:11-12 Musa alimwona Mwebrania akipigwa na wakuu wake wa Kimisri. Musa akawauwa Wamisri. Kimsingi alisukumwa na hasira na huruma.

Fikiria mushtuko wa Musa wakati ndugu zake walipo mgeuzia mgongo kwa kufanya kile alichodhani kilikuwa tendo ambalo lingeweza kuleta ukombozi wao! Mdo. 7:25, "*Alidhani ya kuwa ndugu zake watafahamu ya kuwa Mungu anawapa wokovu kwa mkono wake, lakini hawakufahamu.*"

Hawakuelewa, na wakataka kufahamu aliyemfanya Musa awe hakimu juu yao. Siyo tu kwamba Musa alikataliwa na watu wake mwenyewe, bali pia alikataliwa na Wamisri. Hakika, Farao alijaribu kumwua. Kut. 2:15, "*Basi Farao alipopata habari, akataka kumwua Musa lakini Musa lakini Musa akakimbia mbele ya Farao, akakaa katika nchi ya Midiani; akaketi karibu na kisima.*"

Musa kimsingi alisukumwa zaidi na hisia kuliko ulinganifu. Moyo wake ulikuwa mbele ya kichwa chake. Alikuwa na tabia kama mtu anayetegemea nguvu zake mwenyewe. Baadaye alipaswa kujifunza kwamba ushindi ungepatikana mbali sana kuliko ambavyo angejua. Akiwa na umri wa miaka 40 alimwua Mmisri; akiwa na miaka 80 aliwauwa maelfu kwa msaada wa Mungu.

Kama matokeo ya kukataliwa huku, Musa alikimbilia katika nchi ya Midia. Pale akamwoa binti Jethro, Ziporah. Walikuwa na wana wawili, Geshomu na Eliaza. Alibaki katika nchi ya Wamidia kwa miaka 40.

Hii haikuwa miaka ya hasara. Alikuwa anajiandaa kwa nafasi ya uongozi ambao siku moja ungekuwa wake. Alikuwa mtii katika nidhamu ya jangwa, akijifunza kwanza nchi ambayo angekuwa zaidi sehemu yake.

Miaka arobaini ya tatu

Kut. 3:1-10, "*Basi huyo Musa alikuwa akichunga kundi la Yethro mkwewe, kuhani wa Midiani akaliongoza kundi nyuma ya jangwa, akafika mpaka mlima wa Mungu hata Horebu. Malaika wa BWANA akamtokea katika mwali wa moto uliotokma katikati ya kijiti akatazama, na kumbe kile kijiti kiliwaka moto nacho kijiti hakikuteketea. Musa akasema nitageuka sana, niayaone maono haya makubwa, na sababu kijiti hiki hakiteketei. BWANA alipoona ya kuwa amegeuka ili atazame Mungu akamwita kutoka katikati ya kile kijiti, akasema Musa, Musa! Akasema mimi hapa. Naye asema, usikaribie hapa; vua viatu vyako*

miguuni mwako; maana mahali hapo unaposimama ni nchi takatifu. Tena akasema mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akaficha uso wake; kwa maana aliogopa kumwangalia Mungu. BWANA akasema hakika nimeyaona mateso ya watu wangu walioko Misri, nami nimekisikia kilio chao kwa sababu ya wasimamizi wao; maana nayajua maumivu yao; nami nimeshuka ili niwaokoe na mikono ya Wamisri, niwapandishe kutoka nchi ile, hata nchi njema kisha pana; nchi ijaayo maziwa na asali; hata mahali pa Mkanaani, Mhiti, na Mwamori na Mperizi, na Mhivi, na Myebusi. Basi tazama kilio cha wana wa Israeli kimenifikilia tena nimeyaona hayo mateso ambayo Wamisri wanawatesa. Haya basi, nitakutuma sasa kwa Farao, ili upate kuwatoa watu wangu, hao wana wa Israeli, katika Misri."

Mdo. 7:30-36, "*Hata miaka arobaini ilipotimia malaika wa Bwana akamtokea katika jangwa la mlima wa Sinai katika mwali wa moto, kijitini. Musa alipouona akastajabia maono yale, na alipokaribia ili atazame, sauti ya Bwana ikamjia, mimi ni Mungu wa baba zako, Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Musa akatetemeka asithubutu kutazama. Bwana akamwambia, vua viatu vyako miguuni mwako, kwa maana mahali hapa unaposimama ni nchi takatifu. Yakini nimeyaona mateso ya watu wangu waliomo Misri, nimesikia kuugua kwao nami nimeshuka, niwatoe. Basi sasa, nitakutuma mpaka Misri. Musa huyo waliyemkataa, wakisema ni nani aliyekuweka kuwa mkuu na mwamuzi? Ndiye aliyetumwa na Mungu kuwa mkuu na mkombozi kwa mkono wa yule malaika aliyemtokea katika kile kijiti. Huyo ndiye aliyewatoa akifanya ajabu na ishara katika nchi ya Misri, na katika bahari ya Shamu, na katika jangwa muda wa miaka arobaini.*"

Kutoka katika vifungu hivi tunajifunza kwamba malaika wa Bwana alimtokea katika mwali wa moto katikati ya kichaka. Mungu akanena naye katikati ya kile kichaka. Alimwambia Musa kwamba yeye ni Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo. Mungu alitangaza kwamba watu wake walikuwa wanateswa, na kwamba atawatoa. Musa aliambiwa kwamba anapaswa kusimama mbele ya Farao kwa kusudi la kuwaondoa Israeli kutoka Misri.

Alafu Musa akaanza kutoa udhuru! Mimi ni nani? Kut. 3:11, "*Musa akamwambia Mungu, mimi ni nani hata niende kwa Farao, niwatoe wana wa Israeli watoke Misri?*" Mungu akasema, "*Bila shaka mimi nitakuwa pamoja nawe.*"

Nitasema nini? Kut. 3:13-14, "*Musa akamwambia Mungu tazama nitakapofika kwa wana wa Israeli, na kuwaambia Mungu wa baba zenu amenituma kwenu; nao wakaniuliza jina lake n'nani? Niwaambie nini? Mungu akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO; akasema, ndivyo utakavyowaambia wana wa Israeli; MIMI NIKO amenituma kwenu.*"

Vipi kama hawataamini au kusikia? Mungu akasema kwamba atawapa ishara tatu. Walikuwa na fimbo ambayo ingegeuka nyoka, alafu kulikuwa na mkono uliopooza, na maji ambayo yangegeuka damu (Kut. 4:1-9).

Mimi siyo msemaji mzuri. Mungu akasema atamfundisha Musa cha kusema. Aruni alikuwa msemaji, mara akafanywa msemaji wa Musa (Kut. 4:10-14).

Musa alimfanya Mungu achukie kwa sababu ya udhuru nyingi alizokuwa akizitoa. Kut. 4:13-14, "*Akasema Ee Bwana nakuomba tuma kwa mkono wake huyo utakayemtuma. Hasira ya BWANA ikawaka juu ya Musa, akasema je! Hayupo Haruni, ndugu yako Mlawi? Najua yakuwa yeye aweza kusema vizuri…*"

Mungu akaanza kumweka Musa katika majaribio kwa kusudi la kumsaidia kushinda hisia zake za kushindwa.

- Kut. 4:27-31, "*BWANA akamwambia Haruni nenda jangwani uonane na Musa. Naye akaenda akamkuta katika mlima wa Mungu, akambusu. Musa akamwambia Haruni hayo maneno yote ya BWANA ambayo alimtuma aende nayo, na ishara hizo zote alizomwagiza. Musa na Hruni wakaenda, wakakusanya wazee wote wa watu wa Israeli. Haruni akawaambia maneno yote BWANA aliyonena na Musa akazifanya zile ishara mbele ya watu. Watu wakaamini, na waliposikia ya kuwa BWANA amewajilia wana wa Israeli, na ya kuwa ameyaona mateso yao, wakainama vichwa vyao wakasujudu.*"

- Kut. 6:1-12, "*BWANA akamwambia Musa, sasa utaona nitakavyomtenda Farao; maana kwa mkono hodari atawapa ruhusa kwenda zao, na kwa mkono hodari atawafukuza katika nchi yake. Kisha Mungu aksema na Musa akamwambia, Mimi ni YEHOVA; nami nilimtokea Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, kama Mungu mwenyezi, bali kwa jina langu YEHOVA sikujulikana kwao. Tena nimethibitisha agano langu nao, la kuwapa nchi ya Kanaani; nchi ya kukaa kwao hali ya ugeni. Na zaidi ya hayo nimesikia kuugua kwao wana wa Israeli, ambao Wamisri wanawatumikisha, nami nimelikumbuka agano langu. Basi waambie wana wa Israeli, Mimi ni YEHOVA nami nitawatoa ninyi mtoke chini ya mizigo ya Wamisri, nami nitawaokoa na utumwa wao, nami nitawakomboa kwa mkono ulionyoshwa, na kwa hukumu kubwa; nami nitawatwaeni kuwa watu wangu, nitakuwa Mungu kwenu, ; nanyi mtajua ya kuwa mimi ni YEHOVA, Mungu wenu niwatoaye mtoke chini ya mizigo ya Wamisri. Nami nitawaleta hata nchi ile ambayo naliinua mkono wangu, niwape Ibrahimu, Isaka na Yakobo;*

nitawapa iwe urithi wenu; Mimi ni YEHOVA. Musa akawaambia wana wa Israeli maneno haya, lakini hawakumsikiliza Musa kwa ajili ya uchungu wa moyo, na kwa ajili ya utumwa mgumu. BWANA akasema na Musa akamwambia, Ingia ndani ukaseme na Farao, mfalme wa Misri, ili awape ruhusa wana wa Israeli watoke nchi yake. Musa akanena mbele ya BWANA, akasema tazama hao wana wa Israeli hawakunisikiza mimi; basi huyo Farao atanisikiaje, mimi niliye na midomo isiyo tohara?"

Mifumo ya msingi ilikuwa ni mapigo kumi ambazo Mungu alituma juu ya Misri. Hata kama Haruni alionekana kuwa kiongozi na msemaji kupitia mapigo matatu ya kwanza, Musa akaanza kurekebisha uongozi wake kwa pigo la nne.

Baada ya Waisraeli kuruhusiwa kuondoka, Farao akatuma majeshi ya Misri kuwafuata. Waisraeli walipowaona wana kuja, Musa akasema, "*Simameni imara na muuone wokovu wa Bwana.*" Akainua mkono wake na kunyosha fimbo, na Waisraeli wakapita katika Bahari ya Shamu katika nchi kavu. Majeshi ya Farao walizama majini wakati kuta za maji zilipobomoka.

Vitu vingi vilitokea katika miaka arobaini ya kuzunguka jangwani; mengi sana ya kuonyesha katika somo hili. Lakini Waisraeli walilalamika na kunung'unika sana.

Mara, wale waliokuwa na miaka 20 au zaidi wangeangamia jangwani (Hes. 32:11-12); Yoshua na Kalebo pekee ndiyo waliweza kuingia katika nchi ya ahadi (Hes. 14:22-30)

Musa mwenyewe hakuruhusiwa kuingia katika nchi ya ahadi.

Walipokuwa Kadeshi ya Barinea hawakuwa na maji. Mungu akamwambia Musa kuchukua fimbo yake, akusanye kusanyiko, na anene na mwamba, na maji yangetoka (Hes. 20:1-11)

Musa, akiwa katika hali ya hasira juu ya wana wa Israeli, aksema, "*Lazima tuwachotee maji katika mwamba huu? Alafu Musa akapiga mwamba mara mbili kwa fimbo yake.*" (Hes. 20:10).

Mungu alimwambia Musa na Aruni kwa sababu ya hili hawataruhusiwa kuingia Kanaani. Mungu asingeweza kuangalia yale yaliofanywa na Musa na Haruni kuwatoa wana wa Israeli.

Musa alimsihi Mungu amruhusu kuingia katika nchi. Mungu akasema, "Hapana," lakini alimruhusu kuitazama kwa mbali.

Musa akafa akiwa na miaka 120.

Israeli walilia na kuomboleza juu ya kifo cha Musa kwa siku 30 (Kumb. 34:8).

Kumb. 34:10, "*Hajawai kutokea nabii katika Israeli kama Musa, ambaye BWANA alimjua uso kwa uso.*"